# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**Marking scheme**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

**ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL KCSE**
**TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016**
**102/3**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (i) Mzungumzaji ni Siki, Mzungumziwa ni Diwani IIII, wako nyumbani kwa Diwani III. Wawili hao walikuwa wakizungumzia shida zinazowakumba Wanacheneo na hali mbaya ya uchafu wa kimazingira, Diwani III analamikia hali hii akisema kulikuwa na harufu kila pahali ndiposa Siki anatamka maneno haya.

(ii) **Jadili huka zozote mbili za msemaji zinazojitokeza katika muktadha huu.**

- Ni mtetezi wa haki: Anamtembelea Diwani III kwa lengo la kujadiliana naye kuhusu masaibu yanayowakumba wananchi na jinsi haki zao zinakiukwa na uongozi wa Meya.
- Msema kweli: Anaeleza ukweli kuwa hali ya uchafu mjini ilikuwa imefikia kiwango cha kuvunda.
- Amewajibika: Kwa sababu ameshuhudia maisha duni ya wananchi, anachukuwa jukumu la kumtembelea Diwani III ambaye ni mmojawapo wa viongozi wa baraza la mji ili hatua ichukuliwa ya kutatua matatizo ya wananchi.

(iii) **Thibitisha kuwa Cheneo ilikuwa imejaa uvundo.**

- Kusema kuwa Cheneo ilikuwa imejaa uvundo ni kuashiria kuwa kulikuwa na hali ya uozo katika jamii yenyewe. Jambo hili ladhihirika kwa njia zifuatazo:

a. Kuna visa vya ufisadi: Meya akishirikiana na vibaraka wake kama Bili na Diwani I na II wanapanga njama ya kuuza fimbo ya Meya iliyokuwa mali ya umma kwa lengo la kupata fedha za kujilipa kwa kikao kisicho rasmi. Meya pia anaonekana kumiliki mashamba mengi ambayo ameyapata kwa njia isiyo halali na hata kugawa hizo ploti za umma kwa marafiki wake kama Bili.

b. Meya anasema jinsi alivyomgawia Bili vipande vinne vya ardhi naye baada ya kuuza vipande vitatu amebakisha vitano.

c. Kuna ukatili uliokithiri katika jamii hii: Meya anatumia askari wa baraza kuwatawanya wafanyakazi waliokuwa wakigoma kisha anacheka akifurahia jinsi waandamanaji hao walivyofyatuliwa risasi na wengine katika kufariki.

d. Kuna uchafuzi wa mazingira: kutokana na kuchafuliwa kwa mazingira, kuna uvundo uliosheheni katika eneo hili. Wakati Meya alikuwa akinywa maji anahisi harufu akadhania ilikuwa inatoka majini lakini anaelezwa kuwa uvundo huo ulikuwa ukitokana na takataka.

e. Kuna ubadhirifu wa mali ya umma: Meya na vibaraka wake wanabadhiri mali ya umma kwa kujilipa kwa vikao visivyo rasmi. Walipokuwa na kikao na madiwani wawili na Bili wanapendekeza kuwa wajilipe kwa kufanya kazi ya ziada yaani 'overtime'. Pia Meya anaonekana kutumia mali ya umma na fedha za baraza kujivinjari na marafiki wake kama Bili. Anazungumzza jinzi walivyojivinjari katika hoteli iitwayo Kajifahari pamoja na familia ya Bili.

f. Kuna hali mbaya ya umaskini: Umaskini umekita mzizi katika Cheneo kiasi kwamba kuna watu wasioweza kujinunulia chakula. Mamake Dadavuo Kaole anategemea mabakio ya chakula kumlisha mwanawe. Anasema kuwa mtoto huyo alikula chakula kisichochemshwa kwani hawezi gharamia hata makaa.

g. Kuna hali duni katika mazingira ya kazi: Waridi analalamikia uchafu katika hospitali akisema kwamba nzi walikuwa wanatawala hospitalini.

h. Kuna ukosefu wa huduma muhimu: Hospitali za umma hazina dawa huku viongozi nao wakizidi kutoa ahadi za uongo kwa wananchi wakiwahadaa kwamba dawa hizo zilikuwa zimeagizwa zikiwa bandarini.

i. Kuna unafiki wa kidini: Viongozi wa dini wanatumia dini kujinufaisha. Mhubiri anamwombea Meya aliyekuwa kiongozi dhalimu ili aongoze kwa muda mrefu. Pia anafurahia anapohidiwa kwamba baraza lingelipa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi kando na kugharamia petrol ya kumpeleka kumwombea Meya mara moja kwa juma.

j. Usaliti umekitiri katika jamii hii. Bili anamsaliti Meya kumpotosha kishauri na wakati Meya anashikwa, hajulikani aliko.

1. (i) Tumbo lisilotosheka/matatizo ya tumbo (1 x 2)

(ii) Tarbia – mishororo mine 1 – Kutaja (2)
1 – Kueleza

(iii) Arudhi.
Mishororo mine kila ubeti
Vina vya kati ni, nga
Vipande viwili – ukwapi na utao
Kibwagizo
Mizani – ukwapi (8) utao (8) (4 x 1)

(iv) Lugha nathari
Wapendanao mapenzi yasiyo na dhati wanakuogopa. Wapatao mimba, watoto wao hawajali. Watoto watakapo chakula huwa wanatafuta mapipani. Tumbo nikupe nini ili utosheke? (4 x 1)

(v) Idhini ya mshairi.
Inkisari mf. We – wewe nitakupani
Kuboronga sarufi mf. Wafugaji hata nao – Hata nao wafugaji.
Tabdila mf. Umewasubua – umewasumbua.
Mazida mf. Mnukio – mnuko (2 x 1)

(vi) Kukcsa heshima – hata mbwa wararua.

Ufisadi – hesabu wanazirenga.
Kutowajibikia wana – wanachokora mapipa.
Wizi – wa ng'ombe.
Mizozo/kutoelewana – mradi waliepe njaa. (4 x 1)

(vii) Dibaji – Thibitisha/shalali.
Harara – hasira/hamaki (2 x 1)

2. Vijana kujenga jamii mpya.
   (i) Amani na Imani wanakutana na kuamua kushirikiana licha ya kuwa tofauti.
   (ii) Madhubuti kuungana na tabaka la chini kuleta madbadiliko. Anakangamana na wote na kuhamia kibandani mwa Amani.

   (iii) Amani na madhubuti ambao ni vijana wanahimiza usawa na hivyo kugawia maskini ardhi.

   (iv) Amani na Imani kubadili Imani na mtazamo wa Wanasokomoko kuhusu walemavu/watu wenye mahitaji maalum na kumfanya Majisifu kuenzi wanawe kama binadamu kamili.

   (v) Amani na Madhubuti kusaka haki ya Yusuf na kumtoa gerezani.

   (vi) Amani kukataa kuishi katika nyumba ya Mtemi na kuamua kujenga yake mwenyewe.

   Haja ya bidii.

   (vii) Amani anaamini maridhiano katika jamii baada ya chuki. Anamshawishi Oscar Kambona alilipize kisasi kwa kumuua Mtemi. Pia alimsamehe majisifu kwa kumwibia mswada wake.

   (viii) Madhubuti anapendekeza jamii inayo dumisha maadili. Anakataa kazi anayotafutiwa kifisadi na babake.

   (ix) Imani anabadili taasubi ya kiume kwa kusema kuwa wanawake wasiwekwe pembeni katika kitabu atakachoandika.

   (x) Vijana (Amani) kupinga wizi wa miswada.

   (xi) Amani analeta mfumo mpya wa kuendesha serikali na kuhimiza wananchi wawachunguze viongozi vizuri, wawapige msasa.

   (xii) Amani na Imani wanataka jamii inayomlinda mtoto wanamlea mtoto japo si mtoto wao.

   (xiii) Amani anahimiza uongozi usiwe unafumbiwa macho hata unapokuwa dhalimu.

   (xiv) Amani na Imani kupiga vita Imani potovu ambazo zimepitiwa na wakati mf. Kutokunywa maji ya mto Kiberenge. Zozote 10 x 2 = 20

3. (a) Yalisemwa na Ben Bella.
- Katika barua.
- Kwa mashaka.
- Kuhusu uhusiano wao na sababu ya kuachana. Zozote 4 x 1 = 04

(b) Yaliyojiri.
- Lowela alikuwa mpenziwe Mtemi Nasaba Bora.
- Kwamba alikuwa amempachika mimba.
- Alipelekwa shambani Baraka kufichwa kule.
- Aliificha mimba kwa kufunga kamba tumboni.
- Alijifungua mtoto.
- Alichukuliwa na Mtemi Nasaba Bora na kumweka mlangoni pa Amani.Zozote 4 x 2 = 9

(c)
- Kuacha masomo akiwa mchanga.
- Kukosa nidhamu kwa kujiingiza katika mapenzi nje ya ndoa.
- Kutupa mtoto – Aliikubali achukuliwe.
- Mtoro – Kutoroka nyumbani hivyo kuwasumbua wazazi.
- Anavunja ndoa ya wenyewe. Zozote 4 x 2 = 8

4.
Ulevi – Maeko.
Uzinzi – Samaki wa nchi za Joto.
Ubaguzi – Damu Nyeusi
Tama – Tazamana na Mauti.
Utelekezaji wa watoto – Mzizi na matawi.
Ujambazi – Gilasi ya mwisho makaburini.
Unyanyavaji safi – Samaki wa nchi za joto.
Uanyaji mamba – Samaki.
Upigaji wa wanawake – Maeko, Mwana wa Dorubini.
Uongozi mbaya – kikaza.

5. (a)
- Maelezo ya mwanadishi.
- Kumhusu Sela.
- Alikuwa ametungwa mimba.
- Alifukuzwa shuleni. Zozote 4 x 1 = 4

(b)
- Sela alikuwa mwanafunzi wa kidato cha tatu.
- Alifukuzwa muhula wa tatu.

- Mwalimu Mkuu wa shule ya Timotheo aliita majina ya wasichana watatu.

- Sela alikaa nyumbani kwa muda wa miezi mitatu.

- Sela alimwita Rozina mara tatu. (4 x 1)

(c)
- Masazu anamlaumu Sela kwa kupata mamba.
- Wasichana waliwacheka waliofukuzwa shuleni.

- Majirani wa Mzee Butali waliwacheka.

- Hata waalimu waliona kama ni mzigo wa wale wasichana wenyewe.

(Aeleze dhana ya kanda la usafi na aihusishe katika jibu lake) Zozote 4 x 2 = 08

(d) Umuhimu wa Sela.

- Kielezi cha wasichana wachanga wanaopata mimba kabla ya ndoa.

- Kielelezo cha jinsi wasichana wanavyodanganywa na kulazimika kuacha masomo.

- Mfano mzuri wa majuto. Zozote 2 x 2 = 04

7. Misimu

(a)

(i) Ni maneno au semi zinazozuka katika kindi fulani la watu na huweza kutoweka au kubaki na kusanifishwa kuwa lugha sanifu.

(ii) Umuhimu wa misimu

1. Kuongeza msamati katika lugha.

2. Watu kujitambulisha na kundi fulani.

3. Kupamba lugha ya wanaohisika.

4. Kuburudisha.

5. Kuhifadhi siri.

6. Hukuza utangamano/uhusiano.

7. Hukuza lugha.

8. Huhifadhi utamanduni.

9. Huendeleze historia.

10. Huondoa urasmi katika mazungumzo.

11. Hutafusdi lugha.

(b) Aina za ngomezi za kisasa.

- Rununu.
- Kengele.
- King'ora.
- Mlio wa ambulensi.
- Kipenga.
- Filimbi.

(c) Sifa za maapizo.

- Hutolewa kwa waendao kinyume na maadili ya jamii.
- Huandamana na viapo mbalimbali.
- Yanaweza kutolewa moja kwa moja na anayeathirika au na mtu mwingine kwa niaba yake.
- Huamini wa yataleta maangamizi katika jamii.
- Hutumia lugha kali ya kuogofya.
- Lugha yake ina ufasaha mwingi/ulumbi.

(d)

- Uvumbuzi wa vyombo vya mawasiliano kama tarakilishi.
- Mitambo ya kuchapisha na kuhifadhi maandishi.
- Dini ya Kikristo ambayo inapuuza baadhi ya vitendo au miviga ya F.S.
- Elimu ya kisasa haitambui wala kuthamini F.S.
- Waandishi wengi wa Kiafrika hawashughuliki F.S.
- Vifo vya fanani.
- Ushindani wa F.S. na burundani ya kisasa.